



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA TANDAHIMBA
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)



MKOA WA MTWARA

Simu Na. 023 2410030

Nukushi. 023 2410030

Baruapepe: ded@tandahimbadc.go.tz

Tovuti: www.tandahimbadc.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),

S.L.P. 03,

TANDAHIMBA.

Kumb Na JB.22/124/01B/40

09 Januari, 2024

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Tandahimba anawatangazia waombaji wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya Tandahimba kuleta maombi ya kazi ya Mkataba kwa nafasi iliyoainishwa hapa chini.

MRATIBU WA MFUKO WA ELIMU (NAFASI 1)

Sifa za Mwombaji

Mwombaji anatakiwa awe na shahada katika mojawapo ya fani za ya Utawala na Uongozi, Uchumi, Takwimu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

Mratibu atakuwa na majukumu yafuatayo:

- (a) Kuwa Msaidizi wa katibu wa Mfuko na shughuli za Bodi;
- (b) Kusaidia Kuandaa, kusimamia na kutekeleza mipango na bajeti ya Mfuko wa Elimu;
- (c) Kuandaa taarifa mbalimbali za bodi na kuwasilisha kwa katibu

- (d) Kutunza kumbukumbu, nyaraka na mali za Mfuko wa Elimu wa Halmashauri kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za umma
- (e) Kuratibu na kuhamasisha uchangiaji wa hiari wa Mfuko wa Elimu;
- (f) Kuandaa mipango kabambe ya Halmashauri katika sekta ya elimu ambayo itatilia mkazo mahitaji yote ya elimu katika Halmashauri kwa kuzingatia Mwongozo wa Kitaifa na wa taasisi wa Maendeleo ya Elimu;
- (g) Kuwezesha na kuratibu vikao vya Bodi;
- (h) Kuchambua na kubainisha vipaumbele vya masuala ya elimu katika Halmashauri;
- (i) Kuandaa taarifa za utekelezaji kuhusu Mfuko wa Elimu na maendeleo ya elimu katika Halmashauri.
- (j) Na shughuli nyingine atakazopangiwa na Mwajiri.

Ngazi ya Mshahara

Ngazi ya Mshahara ni TGS D.

MASHARTI YA JUMLA YA MAOMBAJI WA NAFASI ZA KAZI

- a) Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania mwenye Umri kuanzia miaka 18 na wasizidi umri wa miaka 45.
- b) Ajira ya Mkataba wa Mvaka Mmoja.
- c) Waombaji wote wawe tayari kufanya kazi ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba.
- d) Waombaji wote waambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa.
- e) Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, Kidato cha Nne, sita na vyeti vya mafunzo mbalimbali vinavyohusika.
- f) Waombaji wote waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika, pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- g) Waombaji waambatanishe na picha ndogo 2 pasport size zilizopigwa hivi karibuni.
- h) "Testimonials", "*provisional results*", "*statement of results*", Hati ya matokeo ya Kidato cha nne "*result slip*" havitakubaliwa.
- i) Waombaji wenye vyeti vya kidato cha Nne na Cheti cha Taaluma ambao vimepatikana nje ya nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la

Mitihani la Taifa (NECTA), Baraza la Elimu ya Ufundi (NACTEVET),
Tume ya Vyuo Vikuu (TCU).


- j) Waombaji waliofukuzwa kazi, kupunguzwa au kuachishwa kazi katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi.
- k) Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa tu kama wana Kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- l) Watakaochaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili.
- m) Uwasilishaji wa taarifa za kugushi utaadhibiwa kisheria; aidha, maombi yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili au kingereza na yanaweza kuwasilishwa moja kwa moja Masjala ya Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba au kutumwa kupitia posta kwa anuani ifuatayo;

Mkurugenzi Mtendaji (W),

S.L.P 03,

TANDAHIMBA – MTWARA.

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 23 Januari, 2024 saa 9:30 Alasiri


Charles J. Mhaya

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)

TANDAHIMBA

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
S.L.P. Box 03
TANDAHIMBA